



Japani na Tanzania, nusu karne ya kushirikiana kwa maendeleo ya kilimo



Wakulima wakifanya uchunguzi wa masoko.

Mbegu ya karibu miaka 50 ya urafiki kati ya Tanzania na Japan ilipandwa katika mkoa wa Kilimanjaro mnamo mwaka 1974. Kuanzia mwaka huo Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA), lilianza kutekeleza mfululizo wa miradi ya ushirikiano kwa uundaji wa Mpango Jumuishi wa Maendeleo wa Kilimanjaro "Kilimanjaro Region Integrated Development Plan". Baada ya hapo, miradi mbalimbali ya maendeleo ilitekelezwa kama vile "Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Moshi ikifuatiwa na "Kituo cha Kuendeleza Kilimo Kilimanjaro" "Kilimanjaro Agricultural Development Center" (ambacho kwa sasa kinaitwa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro (KATC) "Kilimanjaro Agricultural Training Center".

Shughuli za ushirikiano za

JICA sasa zimesambazwa nchi nzima. JICA inatekeleza mipango miwili katika sekta ya kilimo, ambayo ni:

- i) Mpango wa kusaidia Sekta ya Maendeleo ya Kilimo na
- ii) Mpango wa kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga

i) Programu ya kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo

Kupitia mpango huu, JICA inaendelea kupanua misaada yake kupitia shughuli zake kukabiliana na mahitaji ya kuimarisha na kukuza ongezeko la thamani na kilimo kinacholenga soko, ambayo ni moja ya vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) Awamu ya 2 (2016 / 2017-2025 / 2026). JICA, pamoja na Wizara za Sekta ya Kilimo pamoja na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa

na serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa pamoja zinatekeleza mradi uitwao "Mradi wa Kuimarisha Mpango wa maendeleo wa kilimo wa wilaya (DADP) kupitia Matumizi ya Njia ya SHEP" (TANSHEP) kwa kukuza kilimo kinacholenga soko. Mnamo mwaka wa 2020 tulikamilisha mradi mwingine uitwao "Mradi wa Ukuzaji wa Uwezo juu ya Ukusanyaji wa Takwimu, Uchambuzi na Utoaji wa Takwimu kulingana na ASDP" (Mradi wa ARDS). Mradi huu ulilenga kuimarisha mfumo wa serikali wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E). Sehemu ya kujenga uwezo wa mradi huo sasa imejumuishwa katika mtaala wa Taasisi za Mafunzo za Wizara ya Kilimo ambapo hufundishwa kwa wanafunzi wanaotegemewa kuwa maafisa ugani.

"Anzia Sokoni, Malizia Shambani, Kwa Kipato Zaidi" kaulimbiu ya TANSHEP kubadilisha kilimo kutoka "Kuzalisha na Kuuza" kuwa "Kuzalisha ili Uuze"

Kwa miaka 3 tangu Januari 2019, JICA, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na TAMISEMI wamekuwa wakitekeleza mradi wa TANSHEP ambao lengo lake kuu ni kubadilisha mawazo ya wakulima juu ya kilimo. Kupitia mradi huu, wakulima zaidi sasa wanajifunza jinsi ya kubadilisha mbinu zao za kilimo kutoka "Kuzalisha na Kuuza" kuelekea "Kuzalisha ili Uuze".

TANSHEP imekuwa ikileta mbinu mpya za ugani, uweze-

shaji na ukuzaji wa ukulima mdogomdogo wa mbogamboga (SHEP), kwa jumla ya vikundi 56 vya wakulima wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Wakati kijadi wakulima walitafuta soko baada ya uzalishaji ("Kuzalisha na kuuza"), kwa kupitia njia ya SHEP, wakulima hao sasa hufanya tafti za soko kabla ya kuanza uzalishaji, na kwa kuzingatia utafiti huo wanaamua nini cha kuzalisha, jinsi gani, na lini kulingana na mahitaji ya soko, "Kuzalisha ili Uuze". TANSHEP imewapatia mfululizo wa mipango ya mafunzo ya kiufundi juu ya uchunguzi wa soko, ujengaji wa biashara na wadau, mipango

ya utekezaji na utunzaji wa kumbukumbu za ufuatiliaji na tathmini.

TANSHEP inaweka mbele kaulimbiu hii: "Anzia Sokoni, Malizia Shambani, Kwa Kipato Zaidi." Mmoja wa wakulima, Bwana Joel Jackson Ikeru, ambaye alipewa tuzo ya Mkuu wa Mkoa wa Mkoa Kanda ya Mashariki mwa Tanzania kwa mwaka 2020, aliwaa wakulima wenzekelele kwamba wanapaswa kuangalia soko kwanza kabla ya kuanza uzalishaji, kwa sababu katika soko, wanaweza kujua aina maarufu, ubora na kiwango kinachouzwa, washindani na misimu ya mahitaji ya juu (bei ya juu). Ujumbe huo pia ulitolewa na Waziri wa zamani wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga, katika hotuba yake katika sherehe ya Nane Nane mnamo mwaka 2020, alisisitiza kueneza dhana ya SHEP kote nchini.

Njia ya SHEP sio msaa wa kifedha lakini inatoa fursa kwa wakulima kujua habari na watu kwa biashara yao. Na hii "kujua kitu" inapelekea wakulima kugundua, kuwapa motisha, na kukuza mkakati wa kilimo chao. Kwa mfano, vikundi vya wakulima katika Wilaya ya Karatu, (Migungani, Tujitegemee na Kikundi cha Wakulima cha Migombani) Arusha, ambavyo kijadi walikuwa wanazalisha vitunguu peke yake, viligundua kupitia utafiti wa soko kuwa kulikuwa na mahitaji ya matikiti maji katika masoko ya ndani na gharama ya uzalishaji ilikuwa chini sana kuliko ile ya vitunguu na ina faida. Sasa uzalishaji wao wa mazao umetawanywa ili kukuza uzalishaji wa mbogamboga zenye tija kulingana na mahitaji ya soko na faida. Kwa uuzaji mkakati, TANSHEP inavitaka vikundi vya wakulima kuendelea uchunguzi wa soko kabla ya kuanza uzalishaji na kuendelea kuwasiliana na wanunuzi kujua bei zinazoendelea / zinazotarajiwa hadi kuvuna. Kupitia mchakato huu, wakulima hupata kufikiria kimkakati zaidi



Uvunaji matikitimaji, kikundi cha wakulima cha Migungani Wilaya ya Karatu, Arusha.

2021

Anzia Sokoni Malizia Shambani Kwa Kipato Zaidi

Chukua hatua

Utafiti wa Soko

Januari	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
31	

Julai	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
31	

Agosti	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
31	

Septemba	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
30	31

Oktoba	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
31	

Novemba	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
30	31

Desemba	
Yaliyotokoa	Yaliyotokoa
1	2
3	4
5	6
7	8
9	10
11	12
13	14
15	16
17	18
19	20
21	22
23	24
25	26
27	28
29	30
31	

Mradi wa TANSHEP unatekelezwa na Wizara ya Kilimo ikishirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ufundishaji wa Serikali ya Japani kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). Mradi huu ambao unahamishisha wakulima wadogo wa mazao ya bustani kufanya utafiti wa soko kabla ya kuzalisha, unatekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga kwa muda wa miaka mitano tangu 2019.

KWA WASILIANA:
KATIBU MKUU - WIZARA YA KILIMO, MJI WA SERIKALI, MTUMBA, S.L.P. 2182 DODOMA.
Simu: 255(026) 2321407 Nukushi: 255 (026)2320037. Barua pepe: ps@kilimo.go.tz.
Tovuti: www.kilimo.go.tz.

TANSHEP X Mbwana Ally Samatta

Kalenda ya TANSHEP ikishirikiana na Bwana Mbwana Ally Samatta.



USHIRIKIANO WA JAPAN NA TANZANIA KWA MAENDELEO YA KILIMO



juu ya uuzaji wao. Mfano mzuri ni kikundi cha Mnadani wilayani Lushoto, Tanga, ambacho awali kilipanga kuleta pilipili tamu Dar es Salaam. Kikundi hicho baada ya kufanya utafiti wa soko, mwishowe kilimua kuuza mazao yao katika soko lao, kwani waligundua kuwa bei zilikuwa karibu sawa na zile za Dar es Salaam. Kuuza mazao yao katika masoko ya ndani kulisaidia kupunguza gharama za usafirishaji na kupata faida zaidi.

Hatua kwa hatua lakini kwa kasi, TANSHEP imekusanya ushahidi kwamba mbinu ya SHEP inaweza kufanya kazi ya uboreshaji wa maisha ya wakulima. Kikundi cha wakulima cha Umoja huko wilaya ya Lushoto mkoani Tanga kiliripotiwa kupata faida katika mwaka kwa fedha 2019 / 20 karibu asilimia 30 ya mapato ya jumla kwa kila zao / ekari ikilinganishwa na ile kabla ya kuanza TANSHEP (mwaka 2018 / 19), licha ya ugumu ulioletwa na UVIKO-19. Kikundi cha wakulima cha Nguvu Kazi kutoka wilaya ya Moshi, Kilimanjaro pia kilipata mafanikio ya uzalishaji wa nyanya kwa msimu husika na hivyo kuwezesha washiriki kuanzisha biashara zingine mpya (kama vile ufugaji wa nguruwe).

Ili kutengeneza mafanikio zaidi, juhudi thabiti zinafanywa. Pamoja na TANSHEP, wizara ya kilimo imekuwa ikiangazia njia ya SHEP katika mfumo wa uganu wa kilimo, kupitia marekebisha ya miongozo ya kitaifa ya uganu na mtaala wa mafunzo wa maafisa uganu. Pia imetoa ushauri wa kiufundi kwa walengwa kwa kuhusisha Taasisi ya Utafiti na Mafunzo ya Bustani ya Tengeru (HORTI-Tengeru). TAMISEMI imefanya utaratibu wa kugawana gharama na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA) kwa utekelezaji, wakati wa kuhamasisha Sekretarieti za Tawala za Mikoa (RS) kwa ufuatiliaji wa maeneo husika. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imechangia kuimarisha vikundi vya wakulima kupitia mipango ya mafunzo na ziara za kusoma. Chama cha Kilimo cha Bustani Tanzania (TAHA) kinaipa TANSHEP utaalam wake wa uuzaji na manunuzi kwa mtandao. Kwa kuongezea, mipango kadhaa imeundwa



Mashamba ya Umwagiliaji Mpunga ya Lower Moshi.

katika taasisi zote husika. Kwa mfano, timu za wizara mbalimbali zinazohusika na utoaji na usambazaji habari kwa umma zimekuwa zikizalisha bidhaa mbalimbali za mawasiliano kwa umma ikiwa ni pamoja na kalenda za bango na Mbwana Ally Samatta, mchezaji mashuhuri wa mpira wa miguu, ambaye aliwataka wakulima kujua lengo (masoko), kabla ya kuzalisha (kulima) ambayo ni dhana ya SHEP. Mfano mwingine ni kuanzishwa kwa mfumo wa uthibitisho wa SHEP, ambao unaweza kutoa uthibitisho wa uwezo wa maafisa uganu kwa kuwaongoza wakulima katika kilimo cha kuzingatia SHEP.

ARDS: Taarifa za kilimo zipo tayari kutumika katika kufanya maamuzi ya msingi katika sekta ya kilimo Tanzania

Tangu 2008 mfululizo wa miradi inayolenga kuboresha upatikanaji wa taarifa za kilimo kupitia Mfumo wa Takwimu za Taratibu za Kilimo (ARDS) zilitekelezwa. Kupitia mradi wa ARDS, mtiririko uliwekwa wa taarifa kutoka ngazi ya kata hadi serikali kuu kupitia wilaya na mikoa imeundwa. Takwimu zimesajiliwa na kukusanywa kwenye wavuti, ambayo ni programu ya wavuti iliyoundwa na kutengenezwa kwa kusudi hili maalum, na ripoti zinaweza kuandaliwa kwa urahisi kutokana na taarifa hizo. Hatimaye ARDS inaruhusu watumiaji kupata, kuchakata na kusambaza taarifa za kilimo kupitia programu hii ya tovuti. Kwa kutumia mfumo huu, zaidi ya asilimia 90 ya taarifa za habari

ya kilimo nchini kote zime-wasilishwa kila mwezi tangu mwaka 2017. Kwa kuzingatia kuwa kiwango cha uwasilishaji wa taarifa kama hizo kilisimama kwa 40% mnamo 2015, ni maendeleo ya kustaajabisha katika miaka miwili. Sasa, Wavuti ya ARDS inafanya kazi nchini kote kulipo na muunganisho wa mtandao, na taarifa na ripoti zinazotokana na hiyo zinatumiawa vyema na Serikali (kwa mfano katika Kijitabu cha Kilimo cha Takwimu za Kilimo, kinachoweza kupakuliwa kwenye (<https://www.kilimo.go.tz>))

ii) Mpango wa kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga

Chini ya Mpango huu JICA imesaidia kusambaza teknolojia za kilimo cha mpunga kupitia miradi mbali mbali, yaani Mradi wa Kusaidia Kukuza Sekta ya Mpunga nchini Tanzania (TANRICE2), na Mradi wa Kujenga Uwezo kwa Wataalamu ili Kukuza Maendeleo ya Skimu za Umwagiliaji Chini ya Mipango ya Kilimo ya Wilaya Awamu ya II (TANCAID2), Mradi wa Kuendeleza Skimu za umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP), n.k

TANRICE: Kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga na kuboreshwa kwa mavuno

Kwa karibu nusu karne kuanzia mwaka 1974, JICA na Wizara ya Kilimo nchini Tanzania wamekuwa wakifanya kazi kwa pamoja katika eneo la kuendeleza zao la mpunga. Mfululizo wa miradi ya ushirikiano wa kitaalam imetekelezwa. Mipango mbali mbali ya mafunzo juu ya

kilimo cha mpunga katika kilimo cha umwagiliaji na katika kilimo cha kutegemea mvua ilifanyika kwa maafisa uganu na wakulima kote nchini. Katika programu hizi za mafunzo, wakulima pia walijifunza mada zingine muhimu kama usimamizi wa mfumo wa umwagiliaji, jinsia, masoko, na usimamizi wa zana za kilimo

Jumla ya wakulima 5,235 walipata mafunzo katika miradi 44 ya umwagiliaji kupitia mradi wa ushirikiano wa kitaalam unaoitwa TANRICE (2007-2012). Baadaye, katika awamu ya 2 ya TANRICE 2 (2012-2019), teknolojia na ustadi huu ulisababisha kuongezeka kwa asilimia 40 ya uzalishaji wa mpunga chini ya kilimo cha kutegemea umwagiliaji, ongezeko la asilimia 50 chini ya kilimo cha kutegemea mvua cha mabondeni, na ongezeko la asilimia 140 chini ya kilimo cha kutegemea mvua katika maeneo ya miinuko. Jumla ya wakulima 36,553 na maafisa uganu walipata mafunzo kupitia mradi huo wa TANRICE2.

Programu hiyo pia ilichangia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Mpunga Tanzania (NRDS) ambao ulilenga kuongeza uzalishaji wa mpunga nchini Tanzania kutoka tani 899,000 mnamo 2008 hadi tani 1,963,000 ifikapo 2018 chini ya mpango wa Coalition for African Rice Development (CARD). Lengo la awamu ya pili ya NRDS iliyozinduliwa mnamo mwaka 2019 ni kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza katika uzalishaji wa mpunga, kuchangia utoshelevu wa mpunga katika eneo zima la Afrika, na kuwa kitovu cha

za mradi wa TANCAID2.


Pamoja na maeneo muhimu ya ushirikiano yaliyoonyeshwa hapo juu, kazi za ujenzi wa Mradi wa Maendeleo ya soko la Samaki la Malindi huko Zanzibar ulianza mnamo mwaka 2019.

Kurekebisha soko la samaki la Malindi na Vituo vya uuzaji wa samaki huko Zanzibar

Kupitia msaada wa JICA, mkandarasi wa Kijapani alianza kukarabati soko la samaki la Malindi na Vituo vya uuzaji wa samaki wa Malindi ili kuboresha utoaji wa huduma ili ziwe safi na salama zaidi kwa watumiaji, na hivyo kukuza upatikanaji wa samaki walio bora kwa watu wa Zanzibar. Miundombinu itakayojengwa inatarjiwa kubeba meli za uvuvi, kuleta ajira kwa watu kwenye sekta hiyo, na kuongeza mapato ya wadau katika minyororo ya thamani ya uvuvi na hivyo kukuza uchumi wa bluu wa Zanzibar. JICA inaelewa kuwa uwekezaji wa sekta binafsi ni nguvu nyingine muhimu kwa maendeleo ya nchi. Kwa sababu hiyo kampuni kadhaa za kibinafsi za Japani, zinakuja Tanzania kwa kupitia msaada wa JICA

Utafiti kwa kushirikiana na Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa Ufugaji wa Nyuki nchini Tanzania

Nisshin Honey Co., Ltd ilianzishwa mnamo 1961. Tangu wakati huo, imekuwa ikiendelea biashara yake ya uzalishaji na uuzaji asali nchini Japani. Asali ya Nisshin inashika nafasi ya pili katika sekta ya ufugaji nyuki huko Japani. Kampuni hiyo imekuwa na ufanisi mzuri unaotumia teknolojia ya kisasa, maarifa na uzoefu wa ufugaji nyuki, usafirishaji wa asali na kuchavusha mazao ya monoculture. Nchini Tanzania kampuni hiyo inategemea kuanzisha ubia na kampuni ya hapa nchini ili kuzalisha bidhaa za asali zenye ushindani kwa kuanzisha teknolojia yake ya ufugaji nyuki. Kwa kuanzia kampuni inafanya utafiti juu ya ukusanyaji wa taarifa na kufanya uchambuzi ili kuelewa vyema hali ya sasa katika sekta ya ufugaji nyuki nchini Tanzania kwa kuzingatia mpango wa biashara wa siku zijazo.



Muonekano wa Bandari ya Malindi baada ya mradi kukamilika.



Uvunaji wa asali shambani.